**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
S. L. P. 941,
**DODOMA**

**26 MEI, 2016**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

# *SEHEMU YA KWANZA*

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, napenda kwanza kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili niwasilishe Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii inayohusu Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati hii ndiyo yenye jukumu la kikanuni (Nyongeza ya nane(6) (5) (c) iliyo chini ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kusimamia shughuli za Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi.Aidha, katika Nyongeza hiyo ya Nane, Kanuni ya 7 (1) (a) inaeleza jukumu la Kamati zote za Kisekta ikiwemo Kamati hii la kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia.

Pia kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1-2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kutembelea na kukagua Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ambao ni 2015/2016 pamoja na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha unaoishia ili kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaofuata wa

2016/2017. Lengo ni kuweza kuishauri Serikali namna bora ya kuenenda ili kuleta Maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 14 na 15 Aprili, 2016, Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Dar es Salaam kwa lengo la kupitia na kuchambua Taarifa ya utekelelezaji wa kazi za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 pamoja naMakadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwapunguzia mzigo Watanzania kufuatia agizo lake la kufuta ada na michango mbalimbali katika Elimu ya Msingi na Sekondari. Pamoja na changamoto zilizopo Kamati ina amini Serikali itazifanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo waTaarifa hii umezingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 na hivyo inatoa maelezo ya kina kuhusu masuala manne (4) yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016;
iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
iv) Maoni, Ushaurina Mapendekezo ya Kamati.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIWAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

### 2.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajetikwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilizingatia namna

makusanyo ya Maduhuli yalivyokuwa ikilinganishwa na lengo la kiwango cha ukusanyaji, na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Wizara kama zilivyoainishwa kwenye Mpango wake. Kamati ilipitia Taarifa ya Wizarana kuhoji ili kupata ufafanuzi pale ilipohitajika.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa Bunge lako linapata picha halisi ya ukusanyaji waMaduhuli na upatikanaji wa fedha, Kamati imetumia vielelezo mbalimbali yakiwemo majedwali katika Uchambuzi kwenye Taarifa hii.


### 2.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **263,825,112,771.47,** kati ya hizo shilingi **9,268,463,100**sawa na **asilimia 3.5** zikiwa ni makusanyo ya Wizara na shilingi **254,556,649,671.47**sawa na **asilimi 96.5** zikiwa ni makusanyo kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia Februari, 2016 makusanyo yalikuwa shilingi **181,060,205,382.49** sawa na asilimia **71.1** ya makadirio. Kati ya makusanyo hayo shilingi **4,291,190,118.38** sawa na **asilimia46.2**ya makadirio ya makusanyo ya Wizara yalikusanywa na Wizara na shilingi **176,769,015,264.11** sawa na **asilimia 69.4**ya makusanyo yalikusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara.(***Rejea Kielelezo Na 1).***

***Kamati inaona mwenendo wa ukusanyaji wa Mapato siyo mbaya sana, inaendelea kusisitiza kuwa hadi kufikia Mwisho wa Mwaka wa Fedha 215/2016, Wizara na Taasisi zake zihakikishe ziwe zimefikia lengo na ikibidi livuke.***

**Kielelezo Na.1: UKUSANYAJI WA MAPATO KWA MWAKA 2015/2016**





| | WIZARA | TAASISI | JUMLA |
|---|---|---|---|
| MAKADIRIO | 9,268,463,100 | 254,556,649,671 | 263,825,112,771 |
| MAKUSANYO | 4,291,190,118 | 176,769,015,264 | 181,060,205,382 |

## 2.1.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Wizara hii **(Fungu 46)**iliidhinishiwashilingi **511,525,227,000.00**kwa ajili ya Matumizi ya kawaida. Hadi kufikia robo ya tatu ya Mwaka Machi 2016Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi**316,402,868,828.00**sawa na **asilimia 61.8.**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bajeti ya Maendeleo, Kamati imebaini kuwa katika robo tatu ya Mwaka wa Fedha, Wizara imepokea jumla ya **360,922,754,359.61**sawa na asilimia**61.9**ya fedha iliyoidhinishwa**582,670,597,884.49**.Kamati imebaini kuwa kiasi hiki cha fedha kisichokidhi mahitaji ni moja ya sababu ya kutotekelezwa kwa Miradi ya Maendeleoipasavyo. ***(Rejea Kielelezo Na. 2)***

**Kielelezo Na. 2: UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**



| | ILIYOIDHINISHWA | KILICHOPOKELEWA |
|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | 511,525,227,000 | 316,402,868,828 |
| MIRADI YA MAENDELEO | 582,670,597,884 | 360,922,754,360 |

## 2.2 Maelezo na Matokeo ya Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi waMiradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016. Kamati iliweza kufanya ziara ya Ukaguzi wa Miradi miwili (2) ifuatayo kati ya Miradi iliyotengewa fedha:-

### 2.2.1 Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (**Fungu 46**) iliidhinishiwa **shilingi 418,300,000,000/=** kwa ajili ya Mradi Namba PT4340 uliojulikana kama "***Higher Education Students Loans***" ambao ni Mradi wa kutoa Mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mradihuu ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 7001 - Elimu ya Juu (Higher Education) cha Fungu 46.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ukaguzi huo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto kadhaa kama vile kuchelewa kupokea fedha za Mikopo kutoka Serikalini. Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2016 ambayo ni robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Bodi ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **Bilioni 245** sawa na **asilimia 55.9**tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Fedha hizo zimetumika kutoa Mikopokwajumla ya**wanafunzi 122,786**.***Tafsiri ni kwamba kama fedha hizo zingetolewa zote kwa asilimia 100 basi, wanafunzi wengi zaidi wangepata Mikopo hiyo.***

### 2.2.2 Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifanya ukaguzi waMradi wa Upanuzi na ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS) – Mloganzila. Ujenzi waMradi huu unalenga katika kuboresha Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili kwa kujenga tawi (*Campus*) la Chuo na Hospitali ya kisasa kwa ajili ya kufundishia na kutoa huduma. Tawi hili likikamilika, Chuo kitaweza kuongeza udahili wa

wanafunzi kutoka 4,010 wa sasa hadi kufikia wanafunzi 15,000 jambo ambalo pia litaongeza wataalam wa afya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi ulianza Rasmi mnamo tarehe 10 Machi 2014 na unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 9 Juni 2016. Mradi huu unatokana na mkopo wa riba nafuu kutoka *African Development Bank*(AfDB) wa kiasi cha **dola za kimarekani bilioni 9.4** na mchango wa Serikali ya Tanzania wa **dola za kimarekani 755,000**.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Kamati inatembelea Mradi, ujenzi ulikuwa umefikia asilimia **82.** Hata hivyo, Kamati ilijulishwa pia kiasi cha fedha ambacho kilipaswa kutolewa kama Mchango wa Serikali kilikuwa hakijatolewa***. Ni imani ya Kamati kuwa fedha hizo zitatoka katika Mwaka huu wa Fedha 2015/2016 ili kukamilisha Mradi na kitakachokuwa kimebaki ni ununuzi wa vifaa ambao Kamati ilielezwa umepangiwa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017.***

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa Maoni, Ushaurina mapendekezo yafuatayo kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016:-

a) Kamati imebaini kuwa katika Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili – Mloganzila hakuna fedha iliyotengwa kwaajili ya Ujenzi wa Nyumba za Walimu. Kamati imeshangazwa Mradi mkubwa kama huu kutotengewa fedha za ujenzi wa nyumba za Watumishi na inajiuliza watumishi hawa wataenda kukaa wapi?***Kamati inaitaka Serikali itenge fedha kwaajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi ili Mradi utakapoanza kufanya kazi na nyumba hizo ziwe tayari.***

b) Kamati imebaini kuwa Miradi mingi pamoja na kuwa iliidhinishiwa Fedha katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Lakini haikutekelezwa ipasavyo kutokana na kutopatiwa fedha za kutosha na mingine kutotekelezwa kabisa. ***Kamati inaitaka Serikali kuchagua Miradi michache ya kipaumbele na kuipatia fedha ili iweze kukamilika kwa wakati, ukamilikaji wa Miradi hii utatoa nafasi kwa miaka inayofuata kuendelea na Miradi mingine badala ya kutoa fedha kidogo kidogo au kutokutoa kabisa wakati Miradi imeanza kutekelezwa***.

c) Kamati imebaini pia kumekuwepo na ongezeko la gharama za Miradi kunakotokana na makisio ambayo hufanywa kwa kuzingatia sarafu ya nchi (TSH) wakati Utekelezaji wake unategemea pia sarafu za nchi nyingine.***Kamati inaona kuwa kutokana na ukweli kwamba dola ya kimarekani ndiyo imekuwa ikitumika zaidi kama sarafu ya kufanya manunuzi, ni vyema sasa makisio hayo yakafanyika katika mfumo huo wa dola ili pale dola inapopanda au kushuka isiweze kuathiri Utekelezaji wa Miradi.***

d) Kamati imebaini kuwa vijana wengi wenye alama za kuwawezesha kuendelea na masomo ya elimu ya juu wameshindwa kuendelea kutokana na kutokuwa na uwezo wa kujilipia, uwepo wa Mikopo hii ingekuwa ni fursa njema kwao kujiendeleza kielimu na hivyo kuongeza idadi ya wasomi nchini wenye uwezo wa kuleta tija kwenye Maendeleo ya nchi, ***Kamati imeona ni vyema sasa wanafunzi wengi zaidi waendelee kupewa Mikopo kwa miaka ijayo ili kulifanya Taifa letu kuwa na idadi kubwa ya Wasomi kama zilivyo nchi nyingine ambao watachochea Maendeleo ya endelevu ya nchi. Mchumi Maarufu Duniani na Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Havard Amartya sen aliwahi kusema "Economic growth without investiment in Human Development is unsustainable and unethical".***

## 2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilitoa jumla ya Maoni, Ushauri na mapendekezo 17. Wizara imeweza kutekeleza baadhi ya Maoni hayo na mengine Utekelezaji wake unaendelea.(***Rejea Kiambatisho Na. 1)***

Kamati itaendelea kuyasisitiza Maoni ambayo bado hayajatekelezwailiWizara na Serikali iweze kuyatekeleza kwani ni muhimu sana kutekelezwa kama ilivyopangwa kwa Maendeleo ya Sekta hii na Taifa kwa ujumla.

## *SEHEMU YA PILI*

---

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

### 3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017 Wizara imeainisha jumla ya malengo yake Makuu manne(4) ambayo Kamati ina amini kabisa kama yatafanyiwa kazi ipasavyo ni dhahiri kuwa Wizara hii pamoja na Sekta zake zote zitakuwa na Maendeleo.

### 3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi **(Fungu 46**) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **333,075,815,485.21** ikilinganishwa na kiasi cha shilingi **263,825,112,771.47** zilizokadiriwa katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 ikiwa ni ongezeko la shilingi**69,250,702,713.74**sawa na **asilimia 26.2.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika makadirio ya makusanyo hayo, **kifungu 7001** kinachohusu ***Elimu ya juu*** ndicho chenye makadirio makubwa zaidi yamakusanyo ya Mapato ya shilingi **252,013,955,942.21**sawa na **asilimia75.6** yamakadirio ya makusanyo ya Mapato yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Sababu kubwa ya kuongoza ni kutokana na asili ya kazi zinazofanywa ambazo ni Elimuya Juu kwa hiyo vyuo vyote vipo chini ya kifungu hiki na hivyo ukusanyaji wa ada unachangia kwa kiasi kikubwa ukusanyaji huu wa fedha.

Aidha, katika uchambuzi huo Kamati imebaini kuwa **kifungu 8001** kinachohusu ***Sayansi, Teknolojia na Ubunifu*** ndicho chenye makadirio madogo zaidi ya shilingi **13,565,567,151.00**sawa na **asilimia 4.0**

yamakadirio ya makusanyo ya Mapato yote ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kutokana na asili ya kazi zake na idadi ndogo ya Taasisi zilizo chini yake ambazo ni 5 tu ukilinganisha na 14 za Elimu ya Juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina amini kwamba bado kiwango cha makadirio ya Makusanyo ni kidogo na Wizara inaweza kukusanya zaidi. ***Ni rai ya Kamati kuwa, Motisha itolewe kwa kifungu ambacho kitakusanya zaidi hii itafanya kila kitengo kuongeza juhudi za makusanyo***.

### 3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi


**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara inaomba jumla ya shilingi **1,396,929,798,625.00** Kati ya Fedha hizo shilingi **499,272,251,000.00**sawa na **asilimia 35.7** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **897,657,547,625.00**sawa na **asilimia 64.3**kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kiasi hiki kinachoombwa ni nyongeza ya shilingi **302,733,973,736.51**sawa na **asilimia 27.6** ya kiasi cha shilingi **1,094,195,824,888.49**kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016.***Kamati inaipongeza Serikalikwa ongezeko hili***.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi ili kuona bajeti ya Wizara hii ni sawa na asilimia ngapi ya Bajeti kuu ya Serikali na ilibaini kuwa kiasi hiki kinachoombwa katika Mwaka huu wa Fedha 2016/2017 **NI SAWA NA ASILIMIA 4.4 TU YA BAJETI KUU YA SERIKALI**.***Ipo haja ya kuwekeza zaidi kwenye Elimu kwa kutenga Bajeti ya kutosha kwani Usalama wa nchi tafsiri yake siyo uwepo wa Jeshi Imara tu bali pia Elimubora kwani madhara ya Elimu duni katika usalama wa nchi ni makubwa***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa jumla kuangalia viwango mbalimbali vya Elimu kama uwiano wa idadi ya Walimu na Wanafunzi. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini bado Tanzania tupo nyuma kwani pamoja na kiwango cha Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa na uwiano wa Mwalimu 1 kwa wanafunzi 42 katika Mwaka 2012 na 2013 katika shule za

Msingi, Tanzania bado tuna uwiano mkubwa wa Mwalimu 1 kwa wanafunzi 45 na 43 kwa miaka hiyo 2012 na 2013.(***Rejea Kielelezo Na. 3***)

**Kielelezo Na3. Uwiano waWalimukwa Wanafunzi Shule za Msingi**




| | United Republic of Tanzania | Developed countries | Developing countries | Latin America & the Caribbean | Sub-Saharan Africa | South-Eastern Asia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2010 | 50 | 14 | 26 | 22 | 43 | 21 |
| 2011 | 0 | 14 | 26 | 22 | 43 | 20 |
| 2012 | 45 | 14 | 26 | 21 | 42 | 20 |
| 2013 | 43 | 14 | 26 | 21 | 42 | 20 |

**Chanzo: UNESCO**


## 3.4 Hali ya Elimu Nchini

**Mheshimiwa Spika**, hali ya Elimu nchini kwetu inasikitisha na ni hatari kwa usalama na uhai wa Taifa letu. Tathmini na tafiti nyingi Duniani zimethibitisha Elimu bora ni ile inayoweza kumsaidia raia kukabiliana na changamoto ili kujenga Taifa imara na salama zaidi.Usalama wa nchi huimarika zaidi raia wake wanapoweza kukabiliana na mahitaji ya wakati na jamii husika. Taifa letu limejenga mfumo wa **ELIMU** ambayo haikidhi DIRA **NA MAHITAJI YA NCHI.**Tunahitaji kujenga Taifa la Viwanda lakini hatuna Wataalam wa Hesabu na Sayansi. Dira ya nchi haifungamani na Mkakati wa Elimu, wale wanaofeli ndiyo huandaaliwa kufundisha katika Elimu ya Msingi na Sekondari na wale wanaomaliza Chuo Kikuu wenye wenye ufaulu mzuri wa daraja la kwanza (*1st class*) ndo wanabaki kufundisha vyuo vikuu hili ni jambo la hatari sana kwani Kamati inaona ni sawa na **kujenga msingi wa nyumba mbovu na kumalizia na paa zuri.**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo na ubora wa Elimu kuanzia Mwaka 2005 umekuwa ukishuka kwa kiwango cha kutisha**(*Rejea Kielelezo Na. 4*)**, huu ni

ukweli usiosemwa sana na ambao kama Taifa lazima tuukubali. Toka Mwaka 1961 mpaka leo tumekuwa tukiangalia wingi (Quantity) na siyo ubora (Quality).

**Kielezo Na. 4 : WANAFUNZI WALIOFAULU MITIHANI YA SHULE YA MSINGI NA SEKONDARI KATI YA MWAKA 2005 NA 201**




**Mheshimiwa Spika,** Ualimu umekuwa ni fani isiyo na thamani, umefika wakati sasa kama Taifa kuamua Ualimu na Elimu vipewe thamani yake kwa kutambua kwamba Ualimu siyo chaka la watu waliofeli na wala siyo kazi ya wito bali ni kazi kama ilivyo taaluma nyingine inayotakiwa kuheshimika, kuthaminika kwa kujenga Mfumo wa kutambua na kuboresha Mazingira ya kazi na watoa Elimu.

**Mheshimiwa Spika,** tafiti zimeonyesha kuwa uwezo wa watoto kujifunza kusoma na kuhesabu ni mdogo sana hapa nchini. Kwa mujibu waUtafiti uliofanywa na Taasisi ya Twaweza Mwaka 2014 inakadiriwa kuwa **asilimia 45** pekee ya watoto wa darasa la 3 wanaweza kusoma kwa ufasaha hadithi ya Kiswahili ya darasa la 2, wakati **asilimia 19** pekee ya watoto hao hao wa darasa la 3 wanaweza kusoma kwa ufasaha hadithi ya kingereza ya darasa la 2. Hii ni hatari kubwa sana, Taifa letu linazalisha watumwa na mabwana ndani ya mfumo wetu wa kuendesha, kusimamia na kugharimia elimu, kwa sababu watoto wanaoshindwa kujifunza darasani ni wale wanaotoka familia

masikini, zenye vipato duni na wasiojiweza. Hawa ndio ambao hawawezi kusoma wala kuandika na hata kuhesabu.

**Mheshimiwa Spika**, Utafiti wa Twaweza umebaini pia kuna pengo kubwa kati ya masikini na matajiri katika mfumo wa elimu kwani inakadiriwa kuwa watoto 3 kati ya 10 wenye umri kati ya miaka 13 wanatokea katika familia masikini sana (*ultra-poor households*) ndio walifaulu zoezi la kusoma hadithi za kingereza na kiswahili. Hii maana yake ni kuwa watoto 7 kati ya 10 ya familia masikini zaidi wote hawana uwezo wa kusoma wala kuhesabu. Hii maana yake hawa watakuwa watumwa wa watoto wa matajiri.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya kidato cha nne 2015 yameonesha hali ambayo Serikali na sisi kama Bunge tunatakiwa kuchukua hatua. Shule 50 za kwanza zilizofanya vizuri ni Shule za Binafsi. Matokeo ya aina hii yanathibitisha Dhana aliyowahi kuandika Prof. Marjorie Mbilinyi kuwa **ELIMU BORA** inauzwa na waoto maskini hawatapata Elimu hii. Umefika wakati kama Taifa tukubali uhalisia kuwa **ELIMU BORA** inahitaji uwekezaji na **ELIMU NI UHAI WA TAIFA.** Tusipochukua hatua sasa tutajenga aina mpya ya Ubaguzi kutokana na mfumo wa Elimu wenye tabaka ambalo halitoi **HAKI YA ELIMU BORA KWA MASKINI.**

## ***SEHEMU YA TATU***

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, sasa naomba nitoe Maoni, Ushaurina Mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

### 4.1 Mahusiano ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa takribani **asilimia 80** ya Bajeti ya Serikali inayoelekezwa kwenye Sekta ya Elimu ya Msingi na Sekondari inatekelezwa naOfisi ya Rais –TAMISEMIkutokana na mfumo wa ugatuzi wa madaraka (D by D). Suala hili limekuwa na changamoto katika usimamizi, uendeshaji, udhibiti na ugharamiaji wa mfumo wa elimu nchini. Kwa sasa Sera ipo chini ya Wizara lakini utekelezaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari upo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI. Kamati imebaini pia inapotokea Wanafunzi wameshindwa katika mitihani yao ya kuhitimu anayeulizwa ni Waziri wa Elimuwakatiwaendeshaji, wasimamizi, wagharamiaji wa Elimu kwa maana ya Miundombinu, Walimu na Watendaji wengine wapo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Vile vile, Waziri wa Elimu hana mamlaka juu ya nidhamu, maslahi, mafunzo na usimamizi wa walimu.***Kamati inataka suala hili liangaliwe upya kuepuka Sekta hii kuwa katika usimamizi waWizara zaidi ya moja. Aidha, Sera, usimamizi, uendeshaji, ugharamiaji ufanywe na Wizara ya Elimu na suala la kuendeleza na kusimamia Miundombinu lifanywe na Ofisi ya Rais- TAMISEMI.***

### 4.2 Bajeti

**Mheshimiwa Spika**,Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mara baada ya uhuru aliwahi kutangaza maadui watatu wa Taifa kuwa ni **Ujinga, Maradhi na Umaskini**, hivyo basi hatuna budi kuhakikisha wananchi wanakuwa na Elimu ambayo itawaondoa katika maadui hawa watatu. Hii itawezekana kwakutenga fedha za kutosha ili mazingira ya Elimu yawe ya kuvutia kuanzia mishahara ya Walimu, miundombinu kama

madarasa, mabweni, nyumba za Walimu, maabara na vyoo, vifaa kama vitabu na madawati vyote vinahitaji fedha. Kama ilivyoonyesha awali, Bajeti ya Wizara ya Elimu haiendani kabisa naMpango wa kujikwamua Kielimu. Ni ukweli ulio wazi kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya Elimu, kupunguza umaskini naMaendeleo endelevu.Elimuhubadilisha maisha ya watu kwa kuwawezesha kuwa na ujuzi wa kuboresha maisha yao kwa kujishughulisha katika sekta zilizo rasmi na zile zisizo rasmi.Aliyekuwa Rais wa Afrika ya Kusini Nelson Mandela aliwahi kusema ***"Education is the most Powerful weapon which you can use to change the World" Kamati inaamini kuwaElimu ni silaha muhimu ya kubadilisha Ulimwengu.***Ni kwa msingi huo Kamati inashauri:-

a) ***Serikali iwekeze kwenye Elimu kwaajili ya Maendeleo ya Taifa letu kwa kutenga Bajeti ya kutosha angalau tutimize Azimio la Incheon la kutenga kati ya asilimia 15-20 ya Bajeti kuu ya Serikali kwenye Sekta ya Elimu tofauti na ilivyo sasa ambapo Serikali inatenga asilimia 11.1 tu (Wizara ya Elimu na TAMISEMI)***

b) ***Serikali iangalie namna ya kuweka uwiano kati ya bajeti ya Elimu ya msingi na Elimu ya juu kwani Kamati imebaini kuwa katika fedha za Miradi ya Maendeleo ni asilimia 17 tu ndiyo inatengwa kwaajili ya Elimu ya msingi wakati Elimu ya Juu imetengewa asilimia 48. Ikumbukwe kuwa bila kuwa na msingi imara huku chini elimu ya juu inakuwa haina maana.***

c) ***Bajeti ya Wizara ya Elimu inaonekana kuwa kubwa sana kitarakimu, kiasi cha shilingi trilioni 1.396 na kati ya hizo shilingi bilioni 427.554 sawa na asilimia 30.6 ya Bajeti yote ya Wizarani kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Aidha, bajeti hii ya Bodi ya Mikopo pia ni sawa na asilimia 47 ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii. Hali hii ni inaifanya Wizara kuonekana kuwa na bajeti kubwa sana wakati kiuhalisia si sahihi. Kamati inashauri Fedha za Bodi ya Mikopo kuwa na fungu lake linalojitegemea ili kuweza***

***kuongeza ufanisi wa ufuatiliaji wa Mikopo na kuifanya Bajeti ya Wizara ya Elimu kuwa na uhalisia.***

d) ***Kamati imebaini kuwa Sekta ya Elimu ina taasisi takribani 88 ambazo zinasaidia katika utekelezaji wa majukumu yake. Ambapo inapelekea Taasisi hizo kutumiaasilimia 84% ya bajeti nzima ya Sekta ya Elimu na kufanya Sekta hii kubakiwa na asilimia 16 tu kwa ajili ya kugharimia Maendeleo ya Sekta ya Elimu. Kamati inaona hii sio sawa na hivyo Serikali iweke uwiano mzuri wa fedha kati ya Taasisi na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.***

### 4.3 Elimubila malipo (Waraka Na. 5 wa 2015)

**Mheshimiwa Spika,**Pamoja na maelezo ya ufafanuzi yaliyotolewa na Waziri Mkuu wakati akiwasilisha Bajeti yake kuhusu mahitaji ya msingi ya mtoto (sare za shule na michezo, madaftari, kalamu na chakula, nauli) kuendelea kutolewa na wazaziKamati inatambua changamoto nyingi zilizopo kutokana na waraka huu ambazo Kamati inazitolea Maoni na Ushauri ufuatao:-

a) Miundombinu ya kusomea kamamadarasa, mabweni na vyoo bado havitoshi na hivyo ***Kamati inaitaka Serikali iandae Mpango Mkakati wa haraka wa kuhakikisha inatenga Bajeti Maalum ya kuwezesha miundombinu kupatikanaili suala hili liwe na tija kwani kuongeza idadi ya wanafunzi bila kuboresha miundombinu ni kazi bure. Bajeti ya kiasi cha asilimia 4 tu kati ya bajeti yote ya Sekta ya Elimu kilichotengwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kwa ajili ya Elimu bure kwenye shule za sekondari hakitoshi kabisa na hakina uhalisia katika kugharamia mpango wa elimu bure nchini. Kamati inaitaka Serikali iweke bajeti yenye nia ya dhati ya kutoa elimu bure.***

b) ***Kamati inashauri utekelezaji wa Maoni yaliyopelekwa kwenye Kamati ya Bajeti ikiwa ni pamoja na TEA kupewa fedha***

***zitakazowezesha kujenga Miundombinu ya Elimu hasa madarasa ili kukabiliana na changamoto ya Ongezeko la Wanafunzi***.

c) ***Idadi ya Walimu iongezwe ili kuweza kukabiliana na changamoto ya ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na shule kutokana na hamasa ya wazazi kupunguziwa mzigo.***

d) ***Elimu zaidi iendelee kutolewakwa jamii kuhusu wajibu wa wazazi katika kutekeleza waraka huu waElimu bure***.

### 4.4 Uainishaji wa Vyuo Vikuu (University Classification)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona ni jambo jema nchi kuwa na vyuo vingi kwani ndiyo fursa ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza Elimu ya juu ambao ndiyo wanaotegemewa kuleta Maendeleo ya nchi. Kuwa na vyuo vingi visivyo na ubora na pia kama hakuna uwiano kati ya idadi ya Wanafunzi na ile ya Walimuni kazi bure.

**Mheshimiwa Spika,**Kamati inajiuliza hivi ni nani mwenye jukumu la kuwasimamia Wahadhiri wa Vyuo vikuu hapa nchini? Kamati inauliza hili kwani imebaini kuwa Vyuo hivi vimekuwa vikiongezekawakati Wahadhiri wanaoongezeka ni kidogo sana, matokeo yake unakuta Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndiyo huyo pia anafundisha Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo pia ina maana masomo ya kufundishwa kwa kipindi cha miezi mitatu (3) yanafundishwa kwa muda mfupi zaidi mfano mwezi mmoja (1) au wiki mbili (2)ili kukimbizana na muda. Sio hivyo tu,Kamati inajiuliza tena je nini kinachangia haya yote? Je ni mishahara midogo ndiyo inasababisha Wahadhiri wafanye haya kama njia ya kujiongezea kipato ikiwa ni pamoja na kufanya kazi nyingine nyingi za ushauri ambazo zinachukua muda wao mwingi ambao kiukweli wanapaswa kuutumia kufundisha?

***Baada ya kujiuliza maswali haya, Kamati inapendekeza kuwa:-***

a) ***KwanzaSerikali ifanye uanishaji (classification) ya vyuo hivyo kulingana na kiwango cha ubora wake katika utoaji wa Elimu. Hii itasaidia kuongeza ushindani wa wanafunzi waliopo sekondari na hivyo kusoma kwa bidii. Kamati ina amini kuwa wanafunzi wengi watapenda kusoma chuo chenye sifa ya juu. Kwa mfano Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kikawekewa kiwango cha kufanana na Havard au Yale au Chuo Kikuu cha Dodoma kiwango cha Oxford, n.k.***

b) ***Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha maslahi ya wahadhiri wa vyuo vikuu yanazingatiwa ili kuwaepusha kufanya kazi katika chuo zaidi ya kimoja ili kupata muda wa kutosha kufundisha wanafunzi. Hii iende sambamba na kuongeza idadi ya Wahadhiri ili kuleta uwiano kati yao na wanafunzi.***

## 4.5 Maslahi ya Walimu

**Mheshimiwa Spika,**Maendeleo ya Elimu nchini yanategemea namna Walimu wanavyowezeshwa. Usitegemee Mwalimu ambaye ana manung'uniko ya kutolipwa maslahi yake akafundisha kwa morali. Ukienda nchi nyingine kuwa Mwalimunisuala la kujivunia (*Prestige*), lakini hapa kwetu ualimu sio fani ya kujivunia kabisa imezoeleka kwamba ni wito.Walimu hawaheshimiki yani ni fani ambayo watu wanaenda tu ili mradi maisha yaende. ***Kamati ina amini kuwa fani ya Ualimu ni fani kama fani nyingine. Walimuni nguzo muhimu ya Maendeleo endelevu ya nchina hivyo Serikali haina budi kuwawezesha ili waweze kutoa mchango wao stahiki kwa kuhakikisha maslahi yao yanalindwa kwa kuanzia Kamati inaitaka Serikali kuwalipa madai yao yanayofikia kiasi cha shilingi bilioni 408. Ikumbukwe kwamba viongozi wote tukiwemo sisi Waheshimiwa Wabunge tumepita mikononi mwa Walimu. Kamati inashauri, Serikali kuwalinda, kuwaheshimu na kuwajali walimu wa nchi hii.***

## 4.6 Mfumo wa Elimu

**Mheshimiwa Spika,**Mnamo Mwaka 1981 Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius.K. Nyerere aliunda Tume ya Makwetta ili kuchunguza Mfumo wa Elimu nchini na kutoa Ripoti yake Mwaka 1982 ambayo ilisaidia kuboresha Mfumo wa Elimu nchini ikiwemo uanzishwaji wa Shule za Kata nchini.Aidha, Mwaka 1983 aliyekuwa Rais waMarekani Ronald Regans naye aliunda Tume Maalum ya kuchunguza changamoto ya Mfumo wa Elimu nchini Marekani na namna bora ya kuenenda. Tume hiyo ilikuja na ripoti iliyojulikana '**A Nation at Risk: *The Imperative for Educational Reform'*** ambayo naweza sema ndiyo historia ya mafanikio ya mfumo wa ElimuMarekani.

**Mheshimiwa Spika,** tukiwa Taifa ambalo tunataka kwenda kwenye Uchumi wa Kati yatupasa kujiuliza maswali matano (5) yafuatayojuu ya Mfumo wetu wa Elimu:-

1. Je Maudhui ya Elimu yetu yakoje? Na Je yanazingatia mahitaji ya nchi yetu?
2. Viwango na matarajio, Je ni kwa kiasi gani tupo makini kuhusu upandishaji wa madaraja ilikuwa na viwango vinavyofaa?
3. Muda wa masomo kwa wanafunzi wa shule ya msingi na wale wa Sekondari ukoje, ni masaa mangapi wanatumia kusoma?
4. Maslahi ya Walimu, hapa lazima tujiulize je mishahara ya Walimuinaendana na ushindani wa taaluma yao pamoja na utendaji kazi wao?
5. Rasilimali Fedha: Serikali ina fahamu kuwa ina wajibu wa kusaidia ili kufikia mahitaji ya wanafunzi kama wale waliobarikiwa kuwa na vipawa mbalimbali, walemavu ikiwa ni pamoja na miundombinu yao kwa kuwapa msaada wa fedha lakini pia mafunzo ya utafiti na Elimu ya juu?

**Mheshimiwa Spika,**Baada ya tafakuri hiyo, Kamati inaona ***ni wakati sasa wa kubadili mfumo wa mzima wa Elimu nchini kutoka katika mfumo tulionao wa makundi mawili, kundi la matajiri na kundi la maskini. Kamati inaitaka Serikali kuangalia upya mfumo wetu waElimukwa kuunda TUME MAALUM YA KITAALAM ya kufanya***

***mapitio makubwa ya mfumo wa Elimu nchini na kuchunguza Hali ya Elimu (State of Education)ili kwenda sambamba na kasi kubwa ya mabadiliko ya kiuchumi duniani.Tume hii iwe Tume ya Rais ya kitaalam na Ripoti yake iletwe Bunge ili Bunge nalo lijadili na kutoa mapendekezo ya Kisera, Kisheria kwa Serikali ili kuokoa Elimu yetu.***

***Kamati inashauri Tume hiyo iangalie kuhusu Sera za Elimu; Mfumo wa upatikanaji wa Walimu; Mfumo wa Motisha kwa Walimu; Muda wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Chuo Kikuu; Usimamizi wa Elimu, Uendeshaji na Ugharamiaji wake.***

### 4.7 Tuzo ya Udhamini (*Scholarship Award)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona ni wakati sasa wa kuwekeza kwenye Elimu na kuongeza ushindani kwakutoa tuzo za udhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wamefanya vizuri katika mitihani yao ya Taifa. Kamati inapendekeza tuzo hii iitwe **'Presidential Scholarship Award'*****ambapo wanafunzi 50 watakaofanya vizuri katika mitihani ya kidato cha sita wapewe udhamini wa kusoma katika vyuo bora duniani kama Havard, Yale, Cambridge, Oxford n.k. na wagawanywe katika fani tofauti ikiwemo Sayansi, Uchumi, Sanaa, Siasa n.k.***

**Mheshimiwa Spika**, nchi za Asia ambazo zinajulikana kama 7 ***Asian Tigers*** ukisoma historia yake utagundua karibu zote (Singapore, Malaysia, Korea, Hong Kong, Thailand, Indonesia na Taiwan) ukiacha mambo mengine, ziliwekeza sana kwenye Elimu. Tukiangalia nchi kama Korea ya Kusini mnamo miaka ya 1960 ilikuwa katika Uchumi wa chini zaidi hata ya Tanzania, lakini kwa mujibu wa taarifa kutoka International Monetary Fund (IMF) Mwaka 2015 Korea ilikuwa nchi ya 13 kati ya nchi 180 duniani zenye Pato laTaifa kubwa. Kwa mujibu waMwandishi wa Kitabu kinachoitwa "***Upside –Down Success Story for Korean Economic Development*"** Joong-Kyung Choi ni kwamba Serikali ya Korea ya Kusini iliamua kutoa ufadhili kwa wanafunzi wanaofanya vizuri na wenye vipaji mbalimbali wanatoka katika familia masikini kwenda

kusoma katika vyuo bora duniani katika nchi za Marekani, Ujerumani na Uingereza hali iliyoongeza Wasomi ambao wamesaidia kwa kiasi kikubwa Maendeleo ya Uchumi wa nchi hiyo.

***Kamati ina amini kabisa ufadhili huu utakuwa chachu na utaongeza morali ya wanafunzi kusoma kwa bidii na hatimaye kuwa na Wasomi wazuri wenye taaluma mbalimbali ambazo ni muhimu kwa Maendeleo endelevu ya nchi yetu.***

### 4.8 Mahusiano ya Ongezeko la Idadi kubwa ya watu katika Elimu

**Mheshimiwa Spika**, Mchumi Michael Todaro katika Kitabu chake cha Maendeleo ya Uchumi (*Economic Development 11$^{th}$ Edition*) amebainisha kuwa idadi ya watu duniani imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa na kila Mwaka zaidi ya watu **milioni 75** wanaongezeka na takribani **asilimia 97** ni kutoka nchi zinazoendelea. Aidha, inakadiriwa kuwa hapa nchini kila Mwanamke huzaa wastani wa**watoto 6**. Siyo hivyo tu, takribani **asilimia 44** ya wanawake wanapata mimba ya kwanza wakiwa na umri wa **miaka 19**. Kwa mujibu wa Takwimu za Sensa ya Mwaka 2012 idadi ya watoto kati ya umri wa miaka 2-6 ilizidi wale wa umri wa miaka 10-14 kwa **1,665,843.** Endapo ukuaji huu utaendelea basi **miaka 25** ijayo Serikali itakuwa na mzigo mkubwa ikiwamo kuongeza idadi ya shule pamoja na Walimu kwani idadi ya wanafunzi wanaopaswa kujiunga na Elimu ya msingi itakuwa kwa **333,169** kwa miaka mitano ijayo, na ikiwa kila darasa litakuwa na wanafunzi **40** basi yatatakiwa madarasa mapya **8,392** kwa mwaka na kwa miaka mitano madarasa **41,646**.

***Ni kwa msingi huo :***

a) ***Serikali idhibiti ongezeko la idadi ya watu. Hii itawezekana kwa njia mbalimbali ikiwemo kusomesha zaidi wanawake kwani tafiti zinaonesha kuwa mwanamke anapopata muda zaidi wa kusoma anachelewa kuolewana kuzaa, pia atazaa watoto wachache ambao watakuwa na afya bora lakini pia ambao ataweza kuwasomesha.***

b) ***Serikali iendelee kutoa Elimu ya Uzazi wa Mpango ili kupunguza idadi ya watoto wanaozaliwa kwa kila mwanamke mmoja angalau tufikie wastani wa watoto 3 kwa kila mwanamke.***

c) ***Kamati ina laani vikali wale wote wanaowapa mimba wanafunzi wakiwa shule za Msingi na Sekondari na inaitaka Serikali kuwapa adhabu kali wale wote wanaobainika kufanya vitendo hivi. Aidha, Kamati inaona haina maana kuwafukuza masomo watoto hao wakike na badala yake Kamati inashauri mara baada ya kujifungua wanafunzi hao wapewe nafasi ya kurudi tena masomoni kwa ustawi wao, watoto wao na Taifa kwa ujumla.***

### 4.9 Vyuo vya Ufundi

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuwekeza katika vyuo vikuu, vyuo vya ufundi navyo ni vizuri zaidi katika kuzalisha wataalam wa fani mbalimbali ambao wanasaidia sana katika Mapinduzi ya Viwanda. Dira ya Maendeleo ya 2025 inalenga katika kuibadili Tanzania kutoka katika nchi yenye Uchumi wa chini wa uzalishaji mdogo wa kilimo kwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda na watu wenye Elimu ya Juu. Sasa basi ili kuweza kufikia lengo hilo, ni wakati sasa Serikali kuanza kuweka msisitizo kwenye Elimu ya Mafunzo ya Ufundi ili kuzalisha vijana wenye taaluma na ubunifu ambao utakuwa chachu katika Maendeleo ya Sekta ya viwanda nchini ambayo ni Sekta muhimu katika utoaji wa ajira kwa kufanya yafuatayo:-

a) ***Serikali lazima ihakikishe kila Mkoa una kuwa na vyuo hivi na ambavyo mitaala yake itaendana na mahali. Kwa mfano vyuo vilivyopo kanda ya Ziwa na Pwani ni vyema vikawa na Mitaala ya Uvuvi na vile vilivyopo kwenye Mikoa yenye kilimo kingi basi vikawa na mitaala ya aina hiyo.***

b) ***Kwa kuwa imeonekana kuna Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambavyo havitumiki,Kamati inashauri Serikali ivitumie vyuo***

***hivyo kwa kuvibadilisha kuwa vyuo vya VETA ili kupunguza gharama za ujenzi wa vyuo vipya.***

c) ***Serikali ianzishe Vyuo vya Ufundi (Technical Schools) kama ilivyokuwa kwa Dar Tech, Arusha Tech n.k. Kamati inapendekeza Mikoa kama Kigoma, Mwanza, Rukwa kuwa na vyuo vya ufundi vya aina hii ili viweze kuchochea Uchumi wa Viwanda.***

**4.10 Mamlaka ya udhibiti wa Elimu nchini (Education Regulatory Authority)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kuwa kumekuwepo na Idara ya Ukaguzi wa Elimu katika Wizara hii ambayo ndiyo yenye jukumu la kusimamia ubora wa Elimu nchini. Kamati haikubaliani na Idara hii kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za Idara hii kutokuwa huru lakini pia kutowezeshwa kifedha ili kutekeleza majukumu yake hali ambayo imekuwa ikichangia kushuka kwa viwango vya ubora na ufaulu kutokana na kutokuwepo kwa ukaguzi na ufuatiliaji. Takwimu zinaonesha (BEST 2015) ni **asilimia 19.1** tu ya shule za msingi na **asilimia 21.4** pekee ya shule za sekondari ndizo hukaguliwa kwa Mwaka. Tafsiri yake ni kuwa huichukua Serikali takribani miaka mitano (5) kukamilisha ukaguzi wa shule zote za Umma zilizopo nchini. Au maana yake pia ni kuwa shule hukaguliwa mara moja kila baada ya miaka mitano (5).

***Ni kwa sababu hiyoKamati inaona kuna umuhimu wa kuwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Elimu nchiniambayo itaangalia ubora wa Elimu kuanzia Elimu ya awali hadi Chuo kikuu kwa shule zote za Serikali na Binafsi kwa kuhakikisha Elimu inayotolewa ndiyo ambayo inategemewa hii itasaidia kuwa na kiwango cha Elimu kinachokidhi viwango na ubora. Kwa kufanya hivi tutafikia lengo namba 4 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) linalohusu ubora wa Elimu (Quality Education) ambayo itatutoa katika umaskini huu kama ambavyo Mkurugenzi Mkuu wa UNESCO Bi. Irina Bokova alivyowahi kusema "We know the power of***

***education to eradicate poverty, transform lives and make breakthroughs on all the Sustainable Development Goals,"***

### 4.11 Ada Elekezi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Serikali ipo kwenye mchakato wa kuandaa waraka wa Ada Elekezi kwa shule Binafsi na katika Mwaka huu shule binafsi zimezuiwa kuongeza ada.***Kamati haiamini katika Ada elekezikutokana na ukweli kuwa Serikali imeshakuja na Waraka wake wa kutoa Elimu bure, basi haina budi kuhakikisha Elimu inayotolewa inakidhi viwango hii itasaidia kupanua wigo na hivyo Wazazi wengi watapata nafuu na kuamua kuwapeleka watoto wao katika shule hizo za Serikali na wale watakaopeleka watoto wao shule binafsi basi itakuwa ni kwa utashi wao.***

***Pamoja na hayo Kamati inaitaka Serikali kufanya jukumu lake la kuboresha Elimu kwa kuziwezesha shule za Serikali ili ziwe kama ilivyokuwa zamani kwamba kila mtu alikuwa anatamani kusoma katika shule hizo kama Tabora Boys, Mirambo, Msalato, Kilakala, Pugu, Loleza na nyingine, kutokana na Ubora wa Elimu iliyokuwa inatolewa na Shule hizo.***

### 4.12 Tume ya Utumishi wa Walimu (*Teachers Service Commission*)

**Mheshimiwa Spika,**Kamati imebaini kuwa pamoja na kuunda kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (***Teachers Service Commission***) mnamo Mwaka 2015 ambayo jukumu lake ni pamoja na kuajiri, kupandisha vyeo na kusimamia nidhamu ya watumishi lakini imenyimwa kipengele muhimu cha kulipa mishahara ambayo ingeipa nguvu Tume kwani hakuna sababu ya kuwa Mwajiri wakati hauna jukumu la kulipa Mishahara. Pia, Kamati imebaini kuwa pamoja na Tume hii kusimamia masuala ya Walimu lakini ipo chini ya Ofisi ya Rais - TAMISEMIikiwa imetengewa bajeti ya **shilingi bilioni 10 (Fungu 02)** kwaajili ya uendeshaji. Kutokana na hali hii-

a) ***Kamati inarudia ushauri wake wa kutaka mambo yote yanayohusu Sekta ya Elimu yawe chini ya Wizaramoja ili kupunguza usumbufu huu.***

b) ***Kamati inaitaka Serikali kuipa Tume hii jukumu la kulipa mishahara ili kurahisisha ushughulikiaji wa masuala yote ya walimu na kuwapunguzia usumbufu ambao wanaendelea kuupata.***

c) ***Kutokana na kutokuwa na Bodi ya Taaluma ya Ualimu (Teachers Profession Board) Kamati inaitaka Serikali kuunda Bodi hii ambayo itasimamia Taaluma ya walimu ili kuhakikisha viwango vya Taaluma ya Walimu vinazingatiwa hii itasaidia katika kipindi hiki ambapo kumekuwa na soko huru na hivyo kuwepo kwa walimu wengi ambao wengine hawakidhi viwango vinayotakiwa.***

**4.13 Taasisi ya Elimu Tanzania (Tanzania Education Authority)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kumekuwepo na ucheleweshaji wa upatikanaji wa vitabu katika shule mbalimbali za msingi na sekondari nchini kutokana na Makampuni yanayopewa jukumu la kuandika na kuchapa kuwa na uwezo mdogo.

a) ***Kamati inaitaka Taasisi hii kuliangalia suala hili upya kwa kuwapa Zabuni hiyo Makampuni yenye kukidhi vigezo na viwango ili vitabu hivi viweze kutoka mapema kwani hadi Kamati inakutana na Wizara mwezi Aprili, kuna vitabu ambavyo vilipaswa kuanza kutumika katika Mwaka huu wa masomo vilikuwa bado havijatoka. Kamati inajiuliza wanafunzi hao waliopaswa kufundishwa na kusoma masomo hayo itakuwaje?***

b) ***Kamati inaitaka Taasisi hii kuanza kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya Elimu ya Msingi na Sekondari ya shule za Umma kwa kuipatia fedha za kusaidia Halmashauri katika Ujenzi wa miundombinu.***

### 4.14 Wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wetu waElimu nchini umepitia mambo mengi ya ajabu na ya kusikitishasana. Kama tunavyofahamu, Mamlaka ya Vyuo Vikuu (TCU)inajukumu la kudahiri wanafunzi wenye Elimu ya kidato cha sita na diploma kwa ajili ya kujiunga na Vyuo Vikuu. Katika Mwaka 2013/2014 kuna takribani wanafunzi 1000 waliomaliza kidato cha nnewalidahiriwa na kujiunga na Chuo/Vyuo vikuu. Kamati imeshtushwa na hili na inajiuliza hivi kuna sera yeyote inayoeleza na kuruhusu Mwanafunzi aliyehitimu Kidato cha nne kujiunga na Elimu ya Juu? Na kama ipo ilitungwa lini?Sio hivyo tu bado Kamati inajiuliza je walipewa Mikopona Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu? Kama kweli je ni kwa vigezo vipi?

***Kamati inaona hapa kuna kizungumkuti na hivyo inamtaka Waziri alieleze Bunge lako Tukufu kuhusu suala hili lakini pia afanye uchunguzi kwa Taasisi zote zilizohusika na zichukuliwe hatua za kinidhamu pale zitakapobainika kwamba zilifanya uzembe au kukiuka utaratibu.***

### 4.15 Jengo laElimu

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na utaratibu wa Taasisi nyingi za Serikali zikiwemo za Wizara hii kuamua kujenga majengo yao kwa Matumizi ya Ofisi hata kama taasisi ina watumishi wachache. Kamati inaona ujenzi huu hauna tija na ni gharama kubwa kwa Taifa letu ambalo bado lipo katika listi ya nchi zenye uchumi wa chini.

***Kamati inapendekeza Taasisi zote zilizochini ya Wizarahii kujenga jengo moja litakalojulikana kama ELIMU TOWER na kila Taasisi ikapata Ofisi ndani ya jengo hilo ambayo itapunguza gharama lakini pia itasaidia wadau wanaokuja kupata huduma zinazohusu masuala ya Elimu kuzikuta taasisi zote sehemu moja na hivyo kurahisisha upatikanaji wa huduma.***

## 4.16 Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Mikopo ndiyo moyo wa Taifa hili kwani Mikopo ya Elimu ya Juu imesaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza vyuo vikuu ambalo ni jambo jema sana. Hata hivyo zipo changamoto ambazo Kamati inaona ni muhimu kuzitolea Maoni na Ushauri.

a) Pamoja na lengo zuri la utoaji wa Mikopo kwa wanafunzi, Kamati imebaini kuwa bado watu wengi hawafahamu nini hasa maana ya hii Mikopo na hivyo kuona hawana wajibu wa kulipa mara wanapopata kipato/ajira. ***Kamati inashauri Elimu zaidi iendelee kutolewa kupitia vyombo mbalimbali kama Radio, Magazeti, Televisheni na hata vipeperushi.***

b) Katika kuhakikisha kila mtu aliyepata mkopo anarejesha kwa wakati, ***Kamati inapendekeza Bodi iangalie utaratibu wa kutoa leseni badala ya vyeti mara wanafunzi wanapohitimu na vyeti kutolewa mara baada ya kurejesha mkopo kama nchi nyingine kama vile Uingereza inavyofanya. Mbinu, hii itasaidia Mikopo mingi kurejeshwa kwa wakati na hivyo kuwezesha Wanafunzi wengi zaidi kupata Mikopo. Kwa kuanzia Kamati inashauri kutoa majina ya waliokopa wote kwenye magazeti ya Umma na kupeleka orodha hiyo kwa waajiri wote ili kuwabaini na kuanza kulipa.***

c) ***Kamati inapendekeza kuanzia Mwaka wa Masomo 2016/2017, Wanafunzi wote wanaojiunga na Elimu ya Juu nchini wapewe Vitambulisho vya Taifa vinavyoweza kutambulika na Mabenki ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi mwenye kupata mkopo anaunganishwa na Kitengo cha Uratibu wa Mikopo (Credit Reference Bureau) kilichopo Benki Kuu (BOT) ili kuunganisha Taarifa zake na mabenki na Taasisi nyigine za fedha. Hii itawezesha wanufaika wa mikopo kulipa mikopo hiyokabla ya kupewa mikopo mipya na Benki husika. Kamati inashauri kila mwanafunzi aliyepo kwenye chuo aunganishwe na mfumo huo***

***na hivyo tutakuwa tumemaliza kabisa tatizo la watu kutolipa mikopo yao kwa wakati.***

d) Kutokana na changamoto ya uendeshaji wa Bodi inayotokana na kutojua idadi kamili ya wanafunzi ambao wanapaswa kupata Mikopo kila mwaka,***Kamati inapendekeza kuwa Serikali iamue kuweka idadi kamili ya wanafunzi (fixed number) ya wanafunzi wanaopaswa kupata Mikopo ili Bodi iweze kujipanga tofauti na utaratibu wa sasa wa kutoa Mikopo kulingana na kiwango cha ufaulu***.

e) Kamati ilisikitishwa na changamoto ya ucheleweshaji wa utaoji wa Mikopo kwa wanafunzi ambao wengi wao ni wale wanaotoka kwenye familia duni na hivyo wazazi wao hawana uwezo wa kuwasaidia, ***Kamati inaitaka Bodi ya Mikopo kuanza kutoa Mikopo hiyo kwa wakati ili kuepuka wanafunzi hao kujiingiza katika vitendo visivyofaa kama njia ya kujipatia kipato cha kuweza kujikimu kama vile kufanya biashara ya ngono.***

f) Kamati imebaini kuwa takribani asilimia 48 ya fedha yote ya Miradi ya Maendeleo ya Fungu 46kwa Mwaka huu 2016/2017 ni fedha kwaajili ya Mikopo ya Elimu ya Juu hali inayofanya Bajeti ya Miradi ya Maendeleo kuonekana kubwa wakati kiuhalisia siyo sawa. ***Kamati inashauri kuwa fedha zaMikopo ya Elimu ya juu isiwe sehemu ya Bajeti ya Maendeleo ya Wizara bali iwe ni fedha inayotoka moja kwa moja Hazina (Direct Transfer) au iwe na Fungu lake linalojitegemea.***

### 4.17 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela- Arusha

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi hii ni muhimu sana katika zama hiziza Sayansi na Teknolojia kwani ndiyo inatumika kuendeleza umahiri na weledi katika Maeneo ya Sayansi na Teknolojia*. **Kamati imebaini kwamba Taasisi hii ipo kwenye mpango wa kuanza kufundisha masomo mengine ya Biashara na Utawala kitu ambacho Kamati ina amini halikuwa dhumuni la uanzishwaji wake. Kamati inaona kwa kuwa vipo vyuo***

***vingi vinavyo fundisha masomo haya ya Biashara na Utawala ni vyema Chuo ikaviachia vyuo hivyo kufundisha masomo hayo na chenyewe kikajikita kwenye masomo ya Sayansi na Teknolojia kama lilivyo lengo la uanzishwaji wake ili kuzalisha wataalam tarajiwa.***

**Mheshimiwa Spika*,*** ili kuweza kutoa matokeo tarajiwa***,*** Kamati inaona pia bado Taasisi hii haijawezeshwa vya kutosha ili kutimiza lengo na hivyo ***Kamati inaitaka Serikali kuongeza Bajeti ya Taasisi hii.***


## 4.18 Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Bunge No. 7 ya Mwaka 1986 COSTECH ndiyo chombo pekee cha kutoa ushauri kwaSerikali kuhusu masuala yote yanayohusu Utafiti wa Sayansi na Teknolojia. COSTECH imekuwa ikigharamia Tafiti za kisayansi na kuboresha mazingira ya utafiti ikiwemo miundombinu na vitendea kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika zama hizi za Sayansi na Teknolojia hatuna budi kuhakikisha kwamba Tume hii inafanya kazi ipasavyo. Kamati imebaini kuwa pamoja na umuhimu wa Tume hii lakini bado Serikali haijawa na dhamira ya dhati kuiwezesha ili iweze kutoa matokeo mazuri ambayo ni msingi muhimu kwa Maendeleo ya nchi.Kwa mujibu wa*UNESCO Institute of Statistics* nchi zilizoendelea katika kipindi cha miaka sita (2008-2013) zimekuwa zinatumia wastani wa **asilimia 2.4** ya Bajeti yake ya Matumizi kwa mwaka kwenye Utafiti na Maendeleo wakati nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara zimekuwa zinatumia wastani wa**asilimia 0.4 tu** kwa kipindi hicho. Aidha, kwa mujibu wa Taarifa za Wizara na Vitabu vya Bajeti kiasi kilichotengwa kwaajili ya Mradi wa Utafiti na Maendeleo (*Research and Development*) ulio chini ya COSTECH ni shilingi **Bilioni 10.9 tu** kati ya **Trilioni 23.9** sawa na**asilimia 0.04 tu** ya Bajeti yote ya Serikali kwa Mwaka huu wa Fedha 2016/ 2017, kiasi ambacho ni kidogo sana ukilinganisha na umuhimu wake kwa Maendeleo ya nchi yetu. (***Rejea Kielelezo Na. 4)***

***Kamati inaitaka Serikali kuipatia Taasisi hii fedha nyingi zaidi ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuleta tija.***

**Kielelezo Na.4: % YA FEDHA ZA UTAFITI NA MAENDELEO**




**Chanzo: UNESCO**

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kwa kufanya kazi za Kamati na hususan uchambuzi wa Taarifa kwa weledi wa hali ya juu. Taarifa hii ni matokeo ya kazi yao nzuri ambayo wamekuwa wakifanya kwa kipindi chote tangu Kamati hii imeundwa.

Kwa namna ya kipekee napenda kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Peter Joseph Serukamb, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb | Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Dkt. Charles J. Tizeba, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Peter Ambrose Lijualikali, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Kasuku Samson Bilago, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Dkt. Elly Marko Macha, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Lucia Michael Mlowe, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Dkt. Jasmine Tiisekwa, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Neema William Mgaya, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb | Mjumbe |

14. Mhe. Juma Selemani Nkamia, Mb — Mjumbe
15. Mhe. Seleman Said Bungara, Mb — Mjumbe
16. Mhe. Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mb — Mjumbe
17. Mhe. Boniphace Mwita Getere, Mb — Mjumbe
18. Mhe. Bernadetha Kasabango Mushashu, Mb — Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuliongoza vema Bunge hili la 11.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Waziri waElimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi Pro. Joyce Ndalichako (Mb), Naibu Waziri Eng. Stella Manyanya, Katibu Mkuu Ndg. Maimuna Tarishi, Naibu Katibu Mkuu Prof. Simon Msanjila na Dkt.Leonard Akwilapo pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah kwa ushirikiano mzuri ambao Kamati imekuwa ikipewa. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman B. Hussein, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndg. Dickson M. Bisile pamoja na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Agnes Nkwera na Ndg. Pamela Pallangyo kwa kufanya kazi kwa weledi na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati na Msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John pamoja na Watumishi wote wa Bunge kwa utendaji kazi wao mzuri unaosaidia Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu, likubali na kuridhia kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi (**Fungu 46**) jumla ya shilingi **1,396,929,798,625.00 (Trilioni Moja, Bilioni Mia tatu tisini na sita, Milioni Mia tisa ishirini na tisa, laki saba tisini na nane elfu na mia sita ishirini na tano).**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mussa A. Zungu, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII**

26 MEI, 2016

*KIAMBATISHO NA. 1*

**HOJA ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII KWA MWAKA 2015/2016**

| SN | HOJA / USHAURI | MAJIBU/ MAELEZO |
|---|---|---|
| **UTENDAJI USIORIDHISHA WA IDARA YA UKAGUZI WA ELIMU** | | |
| 5.1 (i) | Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala ya Serikali. | Kwa kuzingatia ushauri uliotolewa na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Wizara imewasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuomba kibali cha kuanzisha Wakala wa Ukaguzi wa Shule kwa barua yenye Kumb. Na. HA.1188/212/03/142 ya tarehe 14 Mei, 2015. |
| 5.1 (ii) | Idara ya Ukaguzi kuongezewa Bajeti. | Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya Idara ya Ukaguzi mwaka hadi mwaka. Katika mwaka wa fedha 2013/14 kiasi cha **shilingi18,308,674,045** kilitengwa, **shilingi 18,792,457,200** zilitengwa mwaka 2014/15 na **shilingi 25,823,307,000** zimetengwa katika mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia **41** ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotengwa 2013/14. |
| **MPANGO WA KUTEKELEZWA KWA MATOKEO MAKUBWA SASA (BRN) KATIKA SEKTA YA ELIMU** | | |
| 5.2 | Serikali ihakikishe kunakuwa na utaratibu wa kupima matokeo ya miradi ambayo inatekekezwa kwa utaratibu wa BRN ili jamii iweze kutathmini mafanikio yanayopatikana na kutofautisha na miradi inayotekelezwa kwa utaratibu mwingine | Ushauri huu umepokelewa na unafanyiwa kazi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2015/2016 serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 4.6 kupitita Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa ajili ya kuwezesha uratibu, ufuatiliaji, uendeshaji na tathmini ya miradi ya elimu ikiwemo miradi ya BRN |
| **MWENENDO WA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA WIZARA NA TAASISI ZAKE** | | |
| 5.3 (i) | Wizara iimarishe ukusanyaji wa maduhuli kwa zile taasisi zake ambazo zimeonesha udhaifu mkubwa katika eneo la ukusanyaji kama Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Mwelekeo wa Serikali kwa sasa ni kuzifanya Taasisi kujiendesha zenyewe kwa kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza vyanzo vya mapato kwa kuendelea kusimamia kwa ufanisi bajeti za mapato, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. |
| 5.3 (ii) | Wizara iangalie namna ya kutumia mfumo wa Kielektroniki katika ukusanyaji na udhibiti wa mapato kwa taasisi zake | Maelekezo ya ukusanyaji na udhibiti wa mapato ya wizara na taasisi kwa kutumia mfumo wa Kielektroniki yamepokelewa. Kwa sasa asilimia kubwa ya makusanyo ya Wizara yanafanywa kupitia benki. |
| 5.3 (iii) | Taasisi ambazo hazikufanya vizuri katika makusanyo ni vyema zikajifunza kutoka kwenye taasisi zilizofikia au kuvuka malengo | Ushauri wa kusisitiza Taasisi kuwa wabunifu na kuongeza makusanyo ya maduhuli umezingatiwa |
| 5.3 | Wizara ibuni vyanzo vipya vya | Mikakati iliyowekwa na Taasisi kubuni vyanzo |

| SN | HOJA / USHAURI | MAJIBU/ MAELEZO |
|---|---|---|
| (iv) | makusanyo ili kuongeza mapato | vingine vya kukusanya mapato (Maduhuli) badala ya kutegemea ada za wanafunzi peke yake ni kama vile kufanya tafiti na huduma za ushauri wa kitaalamu. Aidha kwa taasisi ambazo zinasimamia ubora wa elimu ya juu (TCU na NACTE) zimebuni ada (fee) ambayo inachangiwa na kila mwanafunzi ili kudhibiti ubora wa elimu ya juu nchini. |
| **MKAKATI WA WIZARA KUTEKELEZA VIPAUMBELE** | | |
| 5.4 | Wizara izingatie vigezo vya SMART wakati wa kutekeleza vipaumbele vya majukumu yake | Wizara inatumia Mpango mkakati ambao ni wa mwaka 2014/2015 katika kutekeleza majukumu yake. Mpango huu hutumika pamoja na Mpango wa Kati wa Matumizi ya Bajeti ya Wizara (MTEF) katika kutekeleza vipaumbele vilivyopangwa. |
| **MWENENDO WA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| 5.5 | Serikali iangalie uwezekano wa kutenganisha fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu katika fedha za maendeleo ili kutoa picha halisi ya bajeti ya maendeleo na mwenendo wa utoaji wa fedha hizo kwa miradi husika | Wizara ilikwishapeleka maombi ya kuhamishia tengeo la fedha za Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu kwenda Hazina, hoja hii ilipoletwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii mwaka 2013/2014. Hata hivyo, Hazina waliamua tengeo hili lihamishiwe kutoka katika fedha za Matumizi mengineyo na lijumuishwe kwenye Matumizi ya Maendeleo kama inavyoonekana sasa. Wizara inaiomba Kamati kwa mamlaka yake iishawishi Hazina kuhamisha tengeo hili kama ilivyoagizwa na kamati. |
| **UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015** | | |
| 5.6 (i) | Mradi wa ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe kutopatiwa fedha | Pamoja na kutopatikana kwa fedha kwa mwaka 2014/2015, Serikali imeendelea kutenga fedha za miradi ya maendeleo ambapo katika mwaka fedha 2015/2016 jumla ya shilingi bilioni 1.05 ilitengwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kimetengwa kwa ajili ya kukamilisha mradi huo. |
| 5.6 (ii) | Mradi wa ukarabati na upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kutokamilika kutokana na mkandarasi kutolipwa fedha zake | Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya chuo. Vile vile, katika mwaka wa fedha 2016/2017 kiasi cha shilingi bilioni 4 kimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa chuo kikuu cha Kilimo cha Sokoine.. |

| SN | HOJA / USHAURI | MAJIBU/ MAELEZO |
|---|---|---|
| 5.6 (iii) | Mradi wa ujenzi wa Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutokamilika kutokana na kutopatiwa fedha za maendeleo | Pamoja na kutopatikana kwa fedha katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imeendelea kutenga fedha za miradi ya maendeleo kwa chuo hiki ambapo katika mwaka 2015/2016 chuo kilitengewa jumla ya shilingi bilioni 4 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 kiasi cha shilingi bilioni 5 ilitengwa kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo. |
| **MAFUNZO YA UALIMU KWA VITENDO (BTP)** | | |
| 5.7 | Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo (Block Teaching Practice-BTP) yanafanyika kwa wiki 2 badala ya Wiki 8 kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Kitendo hiki kinaathiri ubora wa elimu. | Kulingana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu, mafunzo kwa vitendo hutolewa kwa namna mbalimbali ikiwemo ufundishaji kiduchu, mafunzo ya muda mfupi ndani ya chuo na ya muda mrefu kwa wiki 8. Wanachuo waliohitimu mafunzo haya mwaka 2015 walifanya mafunzo kwa muda wa wiki 5 (wiki 3 walipokuwa mwaka wa kwanza, wiki 2 walipokuwa mwaka wa pili). Hata hivyo muda huo hautoshi. Muda wa mafunzo kwa vitendo umepungua kutokana na upatikanaji wa fedha hasa kwa mwaka 2013/14 na 2014/15. Ili kuhakikisha kuwa mwalimu mwanafunzi anapata muda wa kupata uzoefu wa kutosha wa mafunzo kwa vitendo, Serikali iliweka zaidi msisitizo kwenye mafunzo ya muda mfupi (mafunzo kiduchu) ili kuhakikisha kiwango cha ubora wa Elimu kinazingatiwa na kinaendelea kukua.<br><br>Aidha, kwa mwaka 2015/16 tengeo limewekwa la kutosha wiki nane. Ikiwa bajeti hii itapitishwa na kutolewa kama zilivyoombwa suala la mafunzo kwa vitendo yatafanywa kwa muda mrefu kama inavyotakiwa. |
| **UKOSEFU WA UFANISI KATIKA MFUMO WA KUHUDUMIA WALIMU (TEACHERS SERVICE DELIVERY SYSTEM)** | | |
| 5.8 (i) | Ni mwingiliano wa majukumu gani unaosababisha mchakato wa kuundwa kwa Bodi ya Kitaalam ya walimu usubiri kuundwa kwa chombo kimoja cha ajira ya walimu? | Kuna mwingiliano wa baadhi ya majukumu kati ya Chombo kimoja cha Ajira ya Walimu na Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ambapo vyombo vyote viwili vina majukumu ya **kusajili** na kushughulikia **nidhamu kwa walimu**. Hivyo Serikali imeona ni busara kuunda kwanza chombo kimoja cha ajira ya walimu na kisha ndipo ikamilishe uundaji wa Bodi ya Kitaalamu |

| SN | HOJA / USHAURI | MAJIBU/ MAELEZO |
|---|---|---|
| | | ya Walimu ili kuondoa mwingilio unaoweza kujitokeza |
| 5.8 (ii) | Serikali iangalie namna ambavyo eneo la huduma za walimu kuwa sehemu ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) | Katika utekelezaji wa mikakati ya mpango wa BRN, kipaumbele namba 9 kinahusiana na walimu. |
| **WALIMU NA MAZINGIRA MAGUMU YA KAZI** | | |
| 5.9 | Walimu waliopo katika mazingira magumu wapatiwe fursa za kujiendeleza wakiwa kazini kwa lengo la kuwajengea uwezo katika taaluma yao | Utaratibu wa walimu kupata nafasi za kujiendeleza upo chini ya utaratibu unaowekwa na mwajiri husika. |
| **UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA VETA** | | |
| 5.10 | Serikali iangalie namna ya kuiongezea uwezo zaidi VETA ili iweze kutimiza wajibu wake kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuvisaidia vyuo vya Maendeleo ya wananchi | Mpango wa ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na OWM – TAMISEMI katika kuvitumia vyuo 55 vya Maendeleo ya wananchi (FDCs) wa kutoa mafunzo ya ufundi stadi yatolewayo na vyuo vya VETA ulianza kutekelezwa Januari, 2013. Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi kati ya 55 vilianza kudahili wanachuo 50 kila chuo na hivyo kufanya jumla ya wanchuo 1,250 kudahiliwa.<br>Mwaka 2013 mamlaka ya VETA ilitoa mafunzo kwa walimu 100 kutoka vyuo 25 vya FDC. Mafunzo yalilenga kuwajengea uwezo walimu waweze kufundisha kwa umahiri fani zilizoainishwa kufundishwa kulingana na makubaliano ya kuanza kutoa mafunzo ya ufundi stadi yatolewayo na vyuo vya VETA katika vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. |
| **UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)** | | |
| 5.11 | Upungufu katika Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Mafunzo ya Ufundi (NACTE) yafanyiwe kazi kuipa mamlaka zaidi ya kusimamia kikamilifu ubora wa mafunzo ya elimu na ufundi stadi nchini | Mapungufu yaliyopo katika Sheria za NACTE yamefanyiwa kazi katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa ajili ya kufanya maboresho ya Sheria hizi. |
| **IDADI YA WANUFAIKA WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU** | | |
| 5.12 (i) | Serikali iangalie namna ya kubuni utaratibu | Ushauri umepokelewa na utafanyiwa kazi na mamlaka husika ili wakati wa kupanga walimu |

| SN | HOJA / USHAURI | MAJIBU/ MAELEZO |
|---|---|---|
| | utakaowawezesha wahitimu wa baadhi ya taaluma kufanya kazi katika maeneo ya pembezoni | wapya wazingatie maeneo ya pembezoni. |
| 5.12 (ii) | Watoto wanaotoka familia duni wapewe mikopo licha ya kuwepo utaratibu wa kutoa mikopo kwa kuzingatia masomo ya vipaumbele. | Ushauri unapokelewa. Aidha, Sheria Na. 9 ya mwaka 2004 iliyorekebishwa mwaka 2007 iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, inataka mikopo kutolewa kwa wanafunzi ambao ni wahitaji. Uhitaji huu hupimwa kwa kuzingatia uwezo wa mwanafunzi kuchangia gharama za elimu ya juu kama Sera ya Elimu ya Juu inavyoelekeza. Utaratibu huu unawezesha watoto wanaotoka familia duni kupewa mikopo hata kama hawasomi masomo ya kipaumbele. |
| 5.12 (iii) | Kuwepo na mkakati wa makusudi wa kukusanya marejesho ya mikopo ya Elimu ya Juu. | Ushauri unapokelewa. Mikakati mbalimbali ya kuwezesha wanufaika wa mikopo kutambuliwa ipo na imekuwa ikitekelezwa na Bodi. Katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Bodi kwa kushirikiana na NIDA inatekeleza mpango wa kuwapatia vitambulisho vya kitaifa wanafunzi wote wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu. Hadi kufikia tarehe 30 Mei,2015 wanafunzi wa vyuo vyote vilivyoko Dar es salaam wameandikishwa na uandikishwaji wa wanafunzi katika vyuo vilivyoko nje ya jiji la Dar es salaam unaendelea. Uandikishaji huu utaiwezesha Bodi kuwatambua kwa urahisi wakopaji hawa baada ya kuwa wamehitimu masomo yao |
| **MPANGO WA MAFUNZO YA KUANDIKA, KUSOMA NA KUHESABU (KKK)** | | |
| 5.13 | Uhitaji wa programu maalum ya mafunzo ya walimu kazini ikiwemo mafunzo ya KKK (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) | Kuna mpango wa kuhuisha Mitaala ya Mafunzo ya Ualimu kawa kuchopeka kipengele cha mafunzo ya KKK ili wahitimu waweze kuwa na weledi mkubwa katika eneo hilo. Aidha, kuna mpango wa mafunzo kazini wa KKK kwa walimu 17,030 wa shule za msingi kutoka katika mikoa 14. Mafunzo hayo yanatarajiwa kuzinduliwa tarehe 07.02.2015 katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na mpango huu ni endelevu. Programu ya mafunzo hayo kwa Mikoa 7 iko chini ya mradi wa EQUIP-T, Mikoa 3 iko iko chini ya UNICEF na Mkoa 1 uko chini ya USAID |
| **WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM** | | |

| SN | HOJA / USHAURI | MAJIBU/ MAELEZO |
|---|---|---|
| 5.14 | Kuwe na Idara kamili inayoshughulika na wanafunzi wenye mahitaji maalum na itakayotengewa fedha za kutosha. | Ushauri umepokelewa Serikali italifanyia kazi ili kuona uwezekano wa kutekeleza ushauri huu. |
| **ELIMU YA JUU KUTENGANISHWA NA ELIMU MSINGI NA SEKONDARI** | | |
| 5.15 | Elimu ya Juu itenganishwe na Elimu Msingi na Sekondari ili kuongeza ufanisi wake. | Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 36 Rais ndiye mwenye mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Jamhuri ya Muungano, ikiwemo uanzishwaji wa Wizara mbalimbali, Idara Zinazojitegemea na Taasisi za Umma. Muundo wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi uliidhinishwa na Rais kwa kuzingatia majukumu ya Wizara. |
| **ELIMU YA WATU WAZIMA KUKOSA MKAKATI WA KUPUNGUZA TATIZO LA KUTOJUA KUSOMA NA KUANDIKA** | | |
| 5.16 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima iwe na mikakati maalum kukabiliana na kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK). | Katika kupambana na tatizo la kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu kuna mipango ifuatayo:<br>1. Kuhuisha mitaala mafunzo ya wataalamu wa elimu ya watu wazima ili wawe mahiri katika kukuza stadi za Kusoma, Kuhesabu na Kuandika (KKK), kuboresha na kuchapa vitabu vya KKK (literacy primers), na kuvisambaza kwa ajili ya kuendeleza watu wazima.<br>2. Kuendelea kutumia wanachuo wa Stashahada wa Elimu ya Watu Wazima kufundisha katika vituo vya elimu ya watu wazima katika mikoa mbalimbali kama sehemu ya mafunzo kwa vitendo ili kusaidia kupunguza uhaba wa walimu wenye weledi wa KKK. Taasisi imeanza na vitua 76 katika Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam na vituo 7 katika Manispaa ya Morogoro.<br>3. Taasisi itashirikiana na Halmashauri za Wilaya katika kufuatilia utekelezaji wa mkakati wa kukuza stadi za KKK katika vituo 10 kila wilaya chini ya mpango wa LANES.<br>4. Kuandaa, kuboresha na kuendeleza kampeni za kisomo<br>5. Taasisi itaendelea kuandaa wataalam |

| SN | **HOJA / USHAURI** | **MAJIBU/ MAELEZO** |
| --- | --- | --- |
| | | watakaosimamia uandaaji na utekelezaji wa mipango ya Elimu ya Watu Wazima katika Mikoa, Wilaya na Kata kupitia mafunzo ya Stashaha na Shahada.<br>6. Kupitia mpango wa Ndio Naweza (YES I CAN), vituo vimefunguliwa na kuwawezesha wanakisomo 3556 kuweza kusoma, kuhesabu na kuandika kuanzia Septemba, 2014 hadi sasa. |
| **MAAZIMISHO YA WIKI YA ELIMU** | | |
| 5.17 | Serikali iendelee kuboresha maazimisho ya wiki ya elimu ili iwe chachu ya kuinua kiwango cha nchini | Suala la kuwatambua wanafunzi na shule zilizofanya vizuri na kutunuku zawadi ni mafanikio ya Wizara na zoezi endelevu. Kupitia maadhimisho ya Wiki ya Elimu kitaifa yanayofanyika kila mwaka kuanzia mwaka 2014, WEMU kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI zimekuwa na utaratibu wa kuwatambua wanafunzi na shule zilizofanya vizuri na kuwazawadia. Kwa mwaka 2015 maadhimisho haya yalifanyika kuanzia tarehe 11 – 15, Mei, 2015 mkoani Dodoma. |